KULEA KIZAZI CHA KESHO KWA AJILI YA MAISHA YA KANISA.

Sehemu ya pili

Mtu,Kuishi na Jukumu la wazazi.

Maandiko:1 wathesaloke 1:5;2Kor 6:1;Yohana1:12-13;1Yoh3:1-2;Wafili 1:19-21a;3:10;Kumbu 6:7;Zaburi 78:5-7,Yoel 1:3;Matendo2:38-39;Waefeso 6:4;2 Tim 1:5;3:15;Wakalatia 6:7-8.

1.Mungu huzingatia sana kile tulicho kuliko yale tuyafanyayo au yale ambayo tunaweza kuyafanya;Anajali sana kujua sisi ni watu wa aina gani na tunaishi maisha ya aina gani-Wathes 1:5;

A.Katika kanisa kitu cha muhimu ni mtu;mtu ndiye njia,na mtu ndiye kazi ya Bwana.-Yohana 5:19;6:57;Wafilipi 1:19-26;Matendo20:18-35;Mathayo 7:17-18;12:33-37.

B.Kichwa cha nyumba huongoza jamii kwa mtu wake;mtu ndiye anayeongoza jamii,wala si kwa mbinu fulani-2Kor6:1,footnote 1;Ufunuo 21:16.

1.Ili kutekeleza jambo lolote,pana haja ya mtu kulifanya;kisha mbinu;hakuna haja ya mbinu nzuri ya utawala;badala yake pana haja ya mtu mzuri kwa ajili ya utawala-Kutoka 4:10,soma footnote 1.

2.Mara tu tunapoanza kujiuzisha na mbinu za kufanya vitu, tunaaanza kuwa wanafiki;Uhalisia wa jambo unamaanisha uthabiti wa jambo ndani na nje-Soma footnote 32:19-21.

11.tunahita kuona ya kwamba sisi ni Mtu-mungu,tumezaliwa na Mungu na wa aina ya Mungu;huu ndio mwanzo wa kuishi maisha ya Mtu-mungu-Yohana 1:12-13;1Yohana 3:2:

A.Tumezaliwa mara ya pili kwa Mungu Roho kufanyika roho-mungu wengi.(Yohana 3:6b)Sisi ni aina ya Mungu; kuuona na kuingia katika ufalme wa Mungu-Yohana1:12-13;3:3,5-6;1 Yohana 3:9.

1.Tukitambua ya kwamba,kama watoto wa Mungu,sisi ni Mungu katika uzima na asili,maisha yetu yatabadilika pakubwa sana ;mazingira na mambo yote yanayotuhusu pia yatabadilika-Yoh 1:12-13;1Yoh 3:2.;

2.Iwapo Wakristo wa leo wote watatambua ya kwamba wao ni Mungu katika uzima na katika asili,ulimwengu wote unaweza kubadilika.

3.Tukifahamu ya kwamba sisi ni mtu-Mungu huu ufahamu,huu utambuzi utatubadilisha katika maisha yetu ya kila siku-Waefeso.4:22-24

B.Tunahitaji kuishi maisha ya mtu-mungu katika maisha yetu ya ndoa-Wafilipi.1:19-21a;3:10

1."Je tunamuishi Kristo katika nyumba zetu tukiwa na waume au wake zetu na pamoja na watoto wetu?Tunahitaji uamsho wa kweli tuwe watu-mungu,wale ambao wanaishi maisha ya kujikana wenyewe na wamesubishwa kumuishi Kristo kwa ajili ya kumthihirisha Mungu"-Life study ya Mambo ya nyakati 1 na 2 ukurasa wa 77.

2."Tunahitaji kuwa waangalifu katika kila jambo maishani mwetu.Kwa mfano mke au mume anapoongea na mwenzake ni lazima tuongee kulingana na roho.Katika mambo yote tunahitaji kuenenda katika roho.(Warumi 8:4).Tunahitaji kuonywa na tuwe makini katika yote tunayo yasema,tunayo yafanya,tunayo yathihirisha,tabia zetu,roho zetu,na makusudio yetu lazima yatakazwe katika roho apeanaye uzima,na roho mjumlifu".-ukurasa wa 49

III.Kando na kitabu cha Mithali ni kana kwamba agano la kale halitupatii mafundisho mengi kuhusu malezi lakini tunayo mifano kadhaa mizuri-Kut.12:3-7;Kumb.6:7-9,20-21;11:18-21;Zab.78:5-7;Yoeli.1:3

A.Adamu na Hawa waliokoka,na wakakabidhi neno la wokovu kwa kizazi kilicho fuata;sisi nasi tunafaa kuyashiriki haya mambo na watoto wetu tukiwaeleza habari ya huzuni kuhusu kuanguka kwa mwanadamu na kuwatangazia habari njema ya uokovu wa Mungu-Mwanzo 3:21;4:4

B."Kwa imani Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora";kwa kuwa Habili alikuwa na imani kama hiyo aliitumia hiyo imani,na akamtolea Mungu dhabihu kulingana na imani hii,huenda alisikia mahubiri ya habari njema kutoka kwa wazazi wake-Wah.11:4

C.Nuhu alirithi njia za kumpenda Mungu kutoka kwa mababu zake;Nuhu alirithi njia ya uokovu ya Adamu,njia ya kutoa dhabihu ya Habili,njia ya Enoshi ya kuliitia Jina la Bwana,na pia njia ya Enoki ya kutembea na Mungu-Mwanzo.3:21,4:4,26;5:22

D.Kumtayarisha Musa,Mungu aliwatayarisha wazazi ambao wamejawa na mawazo ya Mungu baada ya yeye kuzaliwa;kwa kufundishwa na wazazi wake ,Musa alijawa na mawazo na dhana ya Uungu ya kwamba alihitaji kuwaokoa wana wa Israeli-Kut.2:7-9;Wah.11:24-25.

E.Ila Yoshua na Kalebu,wale wote ambao walikuwa wamehitimu na tayari kuingia na kumiliki nchi nzuri walikuwa ni wachanga,kizazi cha pili-Hes.14:29-31,Kumb.1:35-36.

1.Kizazi cha pili hakikuyapitia mafunzo kama yale kizazi cha kwanza kiliyoyapitia,lakini hicho kizazi cha pili kilipokea manufaa na uzoelevu wa kizazi cha kwanza-11:2-7,Yosh.1:1-3.

2.Yale ambayo wazee walipitia yaliwajenga waliyo wachanga na kwa hivyo kutoka katika kizazi cha pili Mungu aliwatayarisha watu laki sita uridhi na msingi imara wa wao kuhitimu na kuundwa kuwa jeshi kwa ajili ya kupigania ufalme wa Mungu-Kumb.1:10-11.

3.Msingi ni uo huo kwetu tuliyo katika urudisho wa Bwana leo hii;yale ambayo wazee wameyaona na kuyapitia yanakabidhiwa walio wachanga na yataweza kuwajenga na kuwatayarisha kupigana pamoja na Mungu na kwa ajili ya Mungu.-2Tim.2:2.

IV.Agano Jipya linazingatia sana mafunzo kwa wazazi na halizingatii sana mafunzo kuhusu kuwa watoto;Waefeso 6 na Wakolosai 3 inatilia mkazo kwa wazazi kuliko kwa watoto-Mat.2:38-39;Waef.6:4,Wako.3:21,2 Tim.1:5;3:15.

A.Tukijumlisha maneno katika Bibilia kuhusu malezi ,kitu cha muhimu ambacho wazazi wanafaa kufanya ni kuwalea watoto wao na kuwahimiza katika Bwana wala si kuwakasirisha au kuwavunja moyo;hii inamaanisha ya kwamba wazazi lazima wajizuie na wasienende katika njia zilizo potovu kwa vyovyote vile-Waefeso.6:4;1 Thes.2:7.

B.Imani ya Timotheo ilikaa kwanza katika nyanya yake,Loisi na katika mama yake Eunike na ilisambazwa hadi kwa Timotheo-2 Tim.1:5;3:15;Waef.6:4.

C.Maria katika sifa zake za kishairi,alinukulu agano La kale ikionyesha ya kwamba Bwana Yesu alilelewa katika jamii ambayo imejawa na elimu na upendo kwa neno la Mungu-Luk.1:46-55.

V.Ni lazima tuone ya kwamba maisha ya Kikristo ni maisha ya kupanda;chochote tunacho kifanya ni aina fulani ya upanzi,aidha kwa mwili au kwa roho-Waka.6:7-8

A.Chochote ambacho tunawaambia na kuwafanyia watoto wetu ni mbegu ambayo tunapanda ndani mwao-footnote 2Tim.3:10

B.Katika maisha ya kanisa,mara kwa mara tunapanda mbegu ndogo;kuwa waangalifu katika kupanda ni kuwa waangalifu katika kuishi kwetu-footnote Waheb.13:7

VI.Kanuni ya Mungu ni ya kwamba baba lazima aishi maisha ambayo ni kielelezo,na ni mfano kwa watoto wake;hata hivyo,lazima tutambue ya kwamba hatima ya watoto wote hutegemea rehema za Bwana-Warum.9:10-13;Waef.6:4.

B.Njia nzuri na bora kuwa wazazi ni kuishi kama mfano kwa watoto wetu na kuomba rehema za Bwana.

C.Iwapo katika kuishi kwetu tunaonyesha mfano mzuri,watoto wetu wakienenda kwa njia mbaya,makosa si yetu;hata hivyo,iwapo hatuwaonyeshi watoto wetu mfano mzuri,tabia mbaya ya watoto wetu itakuwa inatokana na sisi.

D.Ili tuwe mfano mzuri,lazima tumpende Bwana na Neno Lake,tuchukie dhambi,tuchukie utu wetu,na tujifunze mafunzo ya msalaba;huu utakuwa ni mfano mzuri si tu kwa watoto wetu bali pia kwa watakatifu wote.